

**BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI
(NACTE)**

**KUFUNGULIWA KWA MFUMO WA UDAHILI KWA MAFUNZO YA UALIMU
NGAZI YA ASTASHAHADA NA STASHAHADA KWA VYUO VYA SERIKALI NA
VISIVYO VYA SERIKALI KWA MWAKA WA MASOMO 2019/20**

Baada ya kupokea barua ya maelekezo ya udahili na vigezo kwa mwaka 2019/2020 kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) linapenda kuufahamisha umma na wahitimu wa Kidato cha Nne na Kidato cha Sita kuwa nafasi za Mafunzo ya Ualimu ngazi ya **Astashahada** na **Stashahada** kwa mwaka wa masomo 2019/2020 zimefunguliwa rasmi kuanzia tarehe 03/07/2019 hadi tarehe 02/9/2019 na Masomo yanatarajia kuanza mwezi Oktoba, 2019.

Moja ya mikakati ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika kuandaa walimu ni kuhakikisha kuwa wanaojiunga na Mafunzo ya Ualimu ngazi ya Astashahada na Stashahada ni wenye sifa stahiki. Kwa kuzingatia hilo, waombaji wa mafunzo haya ni wenye ufaulu wa Daraja la **Kwanza** hadi la **Tatu** katika mtihamu wa kuhitimu Kidato cha **NNE** (kwa waombaji wa Astashahada (Miaka Miwili) na Kidato cha **SITA** kwa Stashahada (Miaka Miwili). Aidha, kutokana na upungufu mkubwa wa walimu wa **Sayansi na Hisabati**, Lugha, na Biashara kipaumbele kitatolewa kwa waombaji wa Stashahada (Miaka Mitatu) waliofaulu masomo ya Sayansi, Lugha na Biashara kwa alama 'C' katika masomo mawili ya kufundisha (Sayansi/Lugha/Biashara). Aidha, Sifa za kujiunga na programu mbalimbali za Ualimu kwa Vyuo vya Ualimu vya Serikali na visivyo vya Serikali ni kama zilivyoanishwa kwenye **Kitabu cha Mwongozo wa Udahili** (Admission Guidebook) kilichopo kwenye tovuti ya Baraza.

Kwa waombaji wa programu za Ualimu katika **vyuo vya Serikali** watatakiwa kuomba aidha moja kwa moja vyaoni ambako vyuo vitawasajili kupitia '*Institutional Panel*' ya chuo husika au wanaweza kuomba kupitia tovuti ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) (www.nacte.go.tz) kwa kubofya kwenye '*Apply on line (SAVS)*' kisha kufuata maelekezo.

Kwa waombaji kwenye **vyuo visivyo vya Serikali** watatakiwa kuomba moja kwa moja kwenye vyuo husika. Vyuo visivyo vya Serikali vitadahili na kufanya uchaguzi wa wanafunzi wenye sifa na kisha kuwasilisha NACTE majina ya waliochaguliwa kwa ajili ya uhakiki kabla ya kuyatangaza. Vyuo vinaelekezwa kuzingatia utaratibu wa udahili kwa mwaka wa masomo 2019/2020.

Imetolewa na
OFISI YA KATIBU MTENDAJI - NACTE
Tarehe 03/07/2019